

Mjamzito kwa sasa au katika mwaka uliopita?

Pata huduma ya matibabu haraka ikiwa unakumbwa na dalili yoyote kati ya hizi zifuatazo:



Maumivu ya kichwa yasiyokwisha au yanayozidi kuwa mabaya kadiri muda unavyosonga



Kizunguzungu au kuzirai



Mabadiliko katika kuona kwako



Joto la 100.4° F au zaidi



Uvimbe mkubwa sana wa mikono au uso wako



Fikira za kujidhuru au kumdhuru mtoto wako



Matatizo ya kupumua



Maumivu ya kifua au moyo unaopiga kwa kasi




Kichefuchefu kikubwa na kutapika



Maumivu makali ya tumbo yasiyokwisha



Mtoto kuacha kusonga au kupunguza msisimko wakati wa ujauzito



Uvimbe mkubwa, wekundu au maumivu ya mguu au mkono wako



Kutoka damu kwenye uke au kuvuja maji wakati wa ujauzito



Kutokwa damu nzito kwenye uke au kuvuja baada ya ujauzito



Kuchoka kupita kiasi

Hizi zinaweza kuwa dalili za matatizo makubwa sana. Ikiwa huwezi kumfikia mtoa huduma wa afya nenda kwenye chumba cha dharura. Hakikisha unawajulisha kwamba wewe ni mjamzito au ulikuwa mjamzito katika mwaka uliopita.

Jifunze mengi kwenye www.cdc.gov/HearHer



HEAR
SIKILIZA WASIWASI WAKE

Orodha hii ya dalili za tahadhari za dharura kwa kina mama iliundwa na Baraza la Usalama wa Wagonjwa Katika Huduma za Afya ya Wanawake.